MAHUBIRI N°1: HII NDIYO SAUTI YA MATHAYO 25:6

(*Hii mahubiri No1 au "barua ya kimajani", imewekwa kama bahari nyekundu / www.matth25v6.org*)

Kama manabii wa Biblia, mwezi Aprili 1993, mtu mmoja aliyekuwa bado hajaingia kanisa lolote akapata maono, kutembelewa na malaika na huyo akamtuma kwa ujumbe moja kwa ajili ya dunia nzima kwa utimilifu wa huduma ya Mat.25:6 na Ufu.12:14. Shabaha ya kwanza ya ujumbe huu ni: "*…ili kila mtu anayeamini awe na uzima wa milele…*" Sawasawa ilipewa kwa manabii, wachungaji, mitume, wainjilisti na waalimu ulimwenguni kote kuleta miujiza, ufungulifu, na ujuzi duniani kama ilivyosemwa katika Mat.7:21 jinsi inaonekana juu ya vibarua vyao: *"Makesha kuu ya baraka", "Kampeni kuu ya ufungulifu na miujiza", "Makesha kuu ya shukurani na mafanikio katika kazi binafsi", "Seminari kuu ya mafundisho juu ya…", "Makesha kuu ya upako na uponyaji", "Kampeni kuu ya kurudishiwa", "Unashindwa katika ndoa, unafungwa usifanikiwe, una shida fulani*: *kuja!",…*mtu huyu , tarehe 24 aprili 1993 kabla hajaweka mguu wake katika kanisa lolote, alipewa na Mungu kwa wakati wetu (sawasawa Isaya, Yeremia, Ezekieli,…kwa vizazi vyao), siyo tu kuponya na kuleta ufungulifu, lakini kwanza ujumbe utakayoleta uzima wa milele.

Hii ndiyo maono ya wito na utume wake sawasawa alivyo eleza:

WITO NA UTUME

Nimeongoka Aprili 24, 1993 kama alivyoandika Danieli 10:4 mpaka 11 kwa maono ambayo ndani yake nilijikuta wima juu ya mchanga wa bahari, kisha juu ya kichwa cha piramidi ndefu, kisha tena juu ya mchanga wa bahari kwa pahali ingine na nikaona gari kubwa ya kiaskari yenye kuzeeka kutoka kilindi cha bahari na kwenda nyuma yangu. Niligeuka na niliona ilijaa watu wenye uhai. Ilikuwa wanawake na mmoja wao alikuwa mzungu-nusu. Baada ya hayo njiwa wawili wakaja upande wangu kisha tena wakaenda juu ya maji mengi. Kukatokea patwa mwezi (jua). Kisha mtu aliye fanana wingu akishika upanga akashuka toka mbinguni pamoja na Mwana Kondoo moja na dunia ikaangazwa tena. Wakasimama juu ya maji mengi na Mwana Kondoo akaanza kusema nami kwa lugha isiyo julikana. Mlio wa sauti yake ukaingiya ndani mwangu na nikaanguka kama mufu. Nafsi yangu ikaenda kusimama juu ya maji mengi lakini mwili wangu ulilazwa juu ya mchanga wa bahari. Alipomaliza kusema nami, nafsi yangu ikanirudilia na nikawa tena hai lakini sikuwaona tena. Halafu kundi la watu likaja kwangu kutoka upande wa kuume na nikawauliza kama waliona malaika na Mwana Kondoo. Walisema:"Hapana." Na nilisema: Namna gani hamukuona malaika na Mwana Kondoo na yote walifanya? Walijibu: "*Hatukuona malaika na Mwana Kondoo, wala hatukusikia maneno aliyo yasema Mwana Kondoo lakini hakika tunaiamini. Kwa sababu ile tuliyo pewa na Mungu na Shetani akaichukua sasa imekurudishiwa*". Nikanyanyua macho na nikaona kama ngazi imesimamishwa kati ya mbingu na dunia. Na watu wakipanda na kushuka. Maono yakakoma na nikasikia ndani mwangu ile ninayofahamu leo kuwa ni Roho Mtakatifu na nikalia na wakati ule ule nikaamini Mungu.

Kesho baadaye upande wa saa 9 ya mchana, tulipokuwa tumeketi katika jamaa, nikachukuliwa tena katika maono kwa nchi moja iliyo kuwa jangwa na nikaona upande wa mashariki, maneno iliyo shuka toka mbinguni ikichukuliwa juu ya wingu. Ni baada ya maono haya mawili ndipo nilisimama kwenda kanisani mara ya kwanza. [nikisibitishwa hivyo katika utume wa Mathayo 25:6 na Ufunuo 12:14].

Katika ono la tatu, tulikuwa tumeketi ndani ya chumba cha mashindano ya diploma hapo yule aliyekuwa akitujaribu aligawanya barua za mashindano. Nilijiuliza moyoni: "ninafanya hapa nini? Mimi sikufikia hata kiwango cha pili cha masomo na sasa nitaandika nini?[hapo kiwango cha pili: shule ya 2, 1, na shule ya mwisho ya somo kubwa]. Na nyuma kidogo nikaambiwa: "*sawasawa Maria alichukuwa mimba kimiujiza pasipo kujua mume, sawasawa Musa alipata moja kwa moja yaliyopitika kwa uumbaji, umepokea maneno ya uzima wa milele hii tarehe 24 aprili 1993 na hiyo imesimamishwa na Mungu mwenyewe. Wakati itakapotimia utafahamu, na utafundisha yale haukufundishwa ili yeyote anayeamini awe na uzima wa milele".*

JUMBE HUU UNASEMA NINI?

Ujumbe huu unasema kwamba hatuko tena wakati wa jioni lakini katikati ya usiku. Na ni nyakati moja tu na ile ile roho ya Elia lakini ujumbe "mpya" ambayo ni ujumbe wa wakati wa jioni kwa kiwango cha juu sana. [Zakaria 14:7 / Mathayo 25:6].

Ujumbe huu unasema kwamba Baraza la Makanisa Duniani, baraza la kiekumenika kwa makanisa, vyama, miungano , shirikisho na kuhusiana kwa makanisa ... makanisa Katolika, Makanisa ya Kiorthodoksi, Wamethodisti, Ekankar, Horus, makanisa ya Kilutheri, makanisa ya kianglikani, Mahikari, makanisa za ubatizaji, na Rosikrusia, makanisa ya kinazareti , Scientologie, esoterisme, makanisa za kupinga ubatizo, Vodoo, makanisa ya waadventisti, Marafiki wa Yesu, Misioni Emausi, maisha ya kilindi, mashahidi wa Yehova. mashahidi wa Yesu, Kanisa foursquare, Francs-maçons, makanisa ya Pentekoste, na ibada ya miungu Inka, makanisa ya kiprotestanti, Krishna, Kanisa la Kristu, "meditation Transcendentale", "Graal", ya kuita mapepo, makanisa ya kiinjilisti, wamormoni, Guru Maharadji, ... makambi za maombi, "monastères", "couvents", misioni na huduma bila kuacha wabranhamisti [*wale wanaofuata Ujumbe ya William Branham, hata katika ukamilifu wake*] zote ni nyavu za Shetani kwa kupeleka watu jehanamu, na roho inayotenda katika makanisa haya siyo Roho Mtakatifu, lakini mapepo za udanganyifu. Ni zile-zile mapepo zilizokuwa katika mito, mifereji, mask, poro, Vodoo, Dipri, misitu na pori takatifu, asili na desturi ya kiasili na yaliyokuwa yakipandisha wafumu.

Ujumbe huu unasema kwamba ni wale wale mapepo waliyo pandisha Elvis Presley, Bob Marley, James Brown, Madonna, Johnny Haliday, Papa Wemba ni wale wale mapepo wanapandisha leo haya makundi ya wanamuziki wa kiinjili kama Onell Mala, Makoma, ...

Ujumbe huu unasema kwamba T.L. Osborn, Morris Cerullo, Yonggi CHO, Win Worley, Rebecca Brown, Billy Graham, Luis Palau, Frank Alexandre, D. Owens, S. Swingfield, L. Allison, Ewald Frank, Joseph Coleman, Christian Bernard, Jim Lassiter, D.K. Olukoya, Zach. Adetola, Charles Talingano, Benny Hinn, Reinhard Bonnke, ... Kacou Severin, Faustin Shungu, Mamadou Karambiri, Charles Ndifon, Martin Mutyebelé, Derek Prince, Andre Larrue, Yvan Castanou, kākou Gem, Konrad

Raiser, Setri Nyomi, Ayoh Paulo, George Freeman, Cecil Robeck, Theodor Angelou, Hamsa Eichler, Beth Beach Ricardo di Segni, René-Samweli Sirat, JB Nielbien, Nichiko Niwano, Henri Viaud-Murat, Allou Nicolas Yoeli, Honorat Kodjo, Rabbin Schneider , David Rosen, ... wote wanao wafwata nakutumika katika roho moja nao na manabii wote wanao zunguuka nchi ni wachawi na wafumu, pepo wanaotangatanga kwa kazi ya shetani ili wawadanganye wanaokaa duniani, wale ambao majina yao hayakuandikwa katika kitabu cha uzima cha Mwana Kondoo kabla kuweka msingi ya ulimwengu (sawa wakati wa Noa) na huduma yao ni ile ya nyoka (Mwanzo 3, Mathayo 24:24) na ya chura (Ufu.16:13-14) na ya joka. Ni Mungu mwenyewe aliye wapandisha kama jeshi juu ya adui zake (1Fal.22:19-23; 2Thes.2:9-12). Na miujiza yao yote, pamoja na ya wabranhamisti ina shabaha la kudanganya na kuzuiza wateule kutoka Misri na kufanya mugumu moyo wa mafarao na wafalme wao.

Ujumbe huu unasema kwamba makanisa ya Kiprotestanti, kiinjili, misioni na huduma, ni picha ya mnyama, ya Ukatolika, na hii yenyewe ni picha ya Uislamu; na walipokea alama yake, roho yake ambayo wanaita "Roho Mtakatifu". Hata kama wanasema kwa lugha, wanabatiza kwa jina la Yesu Kristo, wanafufua wafu na kuhubiri ukweli, roho zinazo tenda ndani yao ni roho ya chatu, roho ya uchawi. Ujumbe huu unasema kwamba ubatizo wa maji kwa kurudishiwa unalazimishwa kwa wakaaji wa dunia nzima.

Ujumbe huu unasema kwamba Biblia Louis Segond, Tob, Martin, Crampon, Thompson, Scofield, Ostervald, Colombe, semeur, king James, Tmn, na zote zinazo ambatana na hizo, na kati yao ni yote ambayo imerekebishwa; ni vyombo vya uchawi. Na duka za vitabu ziitwazo za kikristo ni picha ya duka za vitabu vya elimu ya mambo ya maarifa na ya uchawi. Na kwamba redio na TV za Kiprotestanti na makanisa za kiinjili kwa mfano wa "frequency vie" ni picha ya redio, TV na gazeti za kikatolika, ni kusema vyombo vya uharibifu na machafuko yote.

Ujumbe huu unahukumu aina zote za shule ya uchungaji. Ujumbe huu unahukumu teolojia [Teo = mungu, lojia =kujifunza] ambayo ni elimu inayo toa msingi wake kuzimuni. Mtu hawezi kujifunza Mungu, wala kujifunza neno lake. Ni Mungu mwenyewe hufunua neno lake na hujifunua kwa yule inampendeza. Ujumbe huu unahukumu kutubu kwa siri[kwa padri ao mchungaji] na unasema tena kwamba kutubu yote inalazimishwa kuwa hazarani, mble ya kusanyiko.

Ujumbe huu unasema kwamba mkataba na kanuni ya upekee kanisani ni Biblia na kwamba kanisa haiwezi kutii serikali na kwa hiyo, hatukubali mamlaka ya "waziri wa ibada" juu yetu.

Ujumbe unasema kwamba hizo FECI, CNEPE-CI ... baraza zote, miungano, na ushirika wa makanisa kwa taifa ao duniani kote ni joka, umbo la shetani wakitumika kwa faida ya shetani.

Siku ya pili ya juma 12 mwezi wa nane 2003, ndugu Filipo alichoma vitabu vyengi, mabarua na kaseti za injili kati yao biblia TOB, Louis Segond, Martin, Ostervald, king james na vitabu vya makaizari Billy Graham, Ewald Frank, Benny Hinn, Reinard Bonnke, T.L. Osborn, kaseti za filme ya "Yesu Mnazareti", sapuli, vieti vya teolojia na vyeti vya mafunzo mbalimbali ya biblia, barua za ubatizo, kaseti za waimbaji wa kidini na wa kipagano,… vitu hivi vimeletwa na wanao amini kelele ya katikati ya usiku kama alivyoandika Matendo ya Mitume 19:18-19. Tangu wakati ule waaminifu wanafanya sawasawa, wakichoma vitu hivi.

Ni ujumbe huu utakaoleta kusanyiko, mateso na kunyakuliwa kwa wachaguliwa lakini ujumbe huu utaenda kwanza dunia nzima. Pia ujumbe huu unaleta ufunuo wa fumbo za mwisho na kutimia kwa ahadi za mwisho za Mungu kwa kanisa la mataifa, ambazo zinapatikana katika Agano la Kale na Jipya, na ambazo ufahamu na kukubaliwa imepewa tu kwa wachaguliwa kama alivyoandika Danieli 12:8-10:"*Wengi watatakaswa na kufanywa weupe, na kusafishwa…wala hakuna mwovu atakayefahamu*", na Matendo 13:48 inasema: "*…na wote waliyokusudiwa kwa uzima wa milele wakaamini".* Na mtu yote anapashwa kufahamu kwamba hakuna awezaye kusimama mwenyewe na kuchoma biblia makumi, kuhukumu na nguvu yote makanisa hizo, viongozi na waamini wao kwa mamlaka iliyo ya Mungu peke. Kwa hivyo, haizuru nani atakaye wazuiza, munalazimishwa kutafuta kujua jambo gani iko ikitendeka kwa sababu hukumuni, kila mtu atajitetea mwenyewe. [tangu mwezi wa nane 2003, haya maandiko (N°1) yamegawanywa kwa uchunguzi wakati wa mahubiri, pamoja na majina ya wachungaji na manabii wa "Cote d'Ivoire". Imewekwa kama kuvuka bahari nyekundu kwa kuingia katika ujumbe. Watakayopita ni peke yao Musa na wayuda kwa mkono wa uwezo wa Mungu. Na kwa ogusti 2006, Roho ilimwambia ndugu Filipo: « *weka mahubiri ya kwanza kwa kipimo cha maandiko ya Biblia na hesabu ya ukurasa utakayopata, ni hiyo urefu na hesabu ya ukurasa kwa ujumbe uliyopewa* »].

MAWASILIANO: Ndugu Filipo:+ 225-0252-0252 E-mail: kacou.philippe@yahoo.fr
Upate mahubiri katika site ya: www.matth25v6.org